Haki zako za Msaada wa Fedha Taslimu na Chakula na Majukumu

Your Cash and Food Assistance Rights and Responsibilities

Jina la Mteja (Mkuu wa Kaya)
Nambari ya Utambulisho wa Mteja:

Majukumu Yako (Unapaswa)

- **Kutupa taarifa tunayohitaji ili kuamua kama unastahiki.**
- **Kutupa uthibitisho pale unapohitajika.** Tunaweza kukupatia. Taarifa unayoipatia idara inategemea uthibitisho wa watumishi wa jimbo na serikali kuu. Uthibitisho unaweza Kujumuisha mawasiliano ya ufuatiliaji kutoka kwa watumishi wa idara wakiwemo wachunguzi wa udanganyifu.
- **Taarifa iliyoripotiwa kwa Idara ya Huduma za Kijamii na Afya** inaweza kuathiri ustahiki wa bima ya huduma ya afya inayosimamiwa na Mamlaka ya Huduma ya Afya na Soko la Ruzuku ya Afya.
- **Kuripoti Mabadiliko** (kwa mfano, anwani, kipato, n.k.) kama inavyotakiwa katika WAC 388-418-0005. Ziripoti hadi ifikapo tarehe 10 ya mwezi ujao.
- **Kushirikiana na Kitengo cha Msaada wa Mtoto (DCS)** kama unakubali msaada wa TANF. Unalazimika kuisaidia DCS kuanzisha, kurekebisha, au kutekeleza msaada wa watoto ambao wapo chini ya uangalizi wako, na kuanzisha nasaba (ikilazimu) kama inavyohitajika katika WAC 388-422-0005. Unaweza kukataa kushirikiana na DCS ikiwa utaweza kuonyesha kwamba una sababu nzuri ya kuamini kwamba kushirikiana na DCS kutakuweka wewe, watoto wako, au watoto ambao wako kwenye uangalizi wako kwenye hatari ya madhara kutoka kwa mzazi asiyekuwa msimamizi
- **Kuomba** na kufanya juhudi za kutosha ili kupata pato linalowezekana kutoka kwenye vyanzo vingine unapoomba au kupokea msaada wa fedha taslimu.
- **Kamilisha ripoti zanazohitajika na mihutasari.**
- **Kufuata masharti ya kazi** kwa ajili ya msaada wa fedha taslimu na msaada wa chakula.
- **Kutujuza** ikiwa unataka mtu mwengine atumie msaada wako wa chakula kwa niaba yako
- **Shirikiana na ukaguzi wetu wa Udhibiti wa Ubora.**
- **Kutumia msaada wa chakula** kwa kununua chakula cha wanakaya wako tu.
- **Kutumia msaada wa fedha taslimu** kwa faida ya wanakaya wako tu.
- **Unalazimika kutoa nambari za Usalama wa Jamii** (SSN) au hali ya uhamiaji kwa watu wanaoomba msaada tu. Kama utachagua kutotoa SSN au hali ya uhamiaji ya wanakaya wasioomba, pato la wanakaya wote na vyanzo bado vitatakiwa kuthibitishwa, kama itahitajika, ili kuamua ustahiki.

Haki Zako (Hatuna Budi)

- **Kupokea maombi** yenye jina lako, anwani, na saini au saini ya mwakilishi aliyeidhinishwa.
- **Kukusaidia kujaza fomu za DSHS.**
- **Kufanyia kazi** ombi lako la msaada wa chakula ndani ya siku 7 ikiwa utakuwa na sifa ya kupata huduma ya haraka.
- **Kukupa risiti** ikiwa utaomba hivyo wakati unapotoa nyaraka.
- **Kukupa maamuzi kwa maandishi**, katika kesi nyingi, ndani ya siku 30.
- **Unaweza kukataa kuongea na mchunguzi wa Upelelezi wa Mapema wa Udanganyifu** (FRED) kutoka Ofisi ya Udanyanyifu na Uwajibikaji. Hulazimiki kumruhusu mpelelezi huyo aingie ndani ya nyumba yako. Unaweza kumwomba mchunguzi aje wakati mwingine. Hili halitaathiri kustahiki kwako kwa msaada.

Haki Zako (Tunapaswa) Inaendelea

- **Unaweza kuomba usikilizwaji kesi wa kiutawala** ikiwa hukubaliani na maamuzi yanayofanywa na idara kwenye kesi yangu. Pia unaweza kumwomba msimamizi au mtawala apitie maamuzi au tendo lenye mgogoro bila kuathiri haki zako za usikilizwaji kesi wa kiutawala.
- **Tunapaswa kukutaarifu** kuhusu kanuni ya miezi 60 ya kikomo cha muda chini ya programu ya Msaada wa Muda kwa Familia Masikini (TANF) na kikomo cha muda chini ya programu ya Msaada wa Fedha taslimu kwa Wakimbizi (RCA), ambayo huanza tangu tarehe utakapokuwa unastahiki kupata ruzuku za wakimbizi kwa mara ya kwanza. Ikiwa tarehe hiyo ni tarehe 5 Mei, 2025 au baada yake, kikomo cha muda ni miezi minne (4). Ikiwa tarehe hiyo ni kabla ya tarehe 5 Mei, 2025, kikomo cha muda ni miezi 12. Kikomo hichi cha muda hakitumiki kwenye Chakula chako cha Msingi, au ruzuku za uangalizi wa mtoto.

Mambo Unayopaswa Kujua Kuhusu Kadi Yako ya EBT

- **Matumizi Mabaya ya Ruzuku:** Ruzuku za chakula na fedha taslimu zinazosambazwa kupitia kadi ya EBT zitaipa DSHS historia ya kumbukumbu kuhusu ulipotumia ruzuku zako. Idara itatumia taarifa ya kumbukumbu kwenye uchunguzi wa matumizi mabaya ya ruzuku za msaada wa fedha taslimu au kubadilishana kwa ruzuku za msaada wa chakula kwa fedha au vitu vingine vya thamani (biashara haramu).
- **Ubadilishaji wa kadi ya EBT:** Tunaweza kudai malipo ya ubadilishaji wa kadi za EBT Tunza kadi yako ya EBT na namba ya kitambulisho chako (PIN).
- **Akiba Kubwa ya Kadi za EBT:** Ikiwa itatokea hutatumia ruzuku zako kwa miezi au ukalimbikiza akiba kubwa baada ya miezi kadhaa, tunaweza kuwasiliana na wewe ili kukagua hali yako au mahitaji yako ya ruzuku.

Mambo Unayopaswa Kujua (Chakula cha Msingi)

- **Tutatuma taarifa** kwenda wakala nyingine za serikali kuu kuhusu mtu anayeomba Chakula cha Msingi ili kuangalia kama taarifa ni sahihi. Ikiwa taarifa yoyote sio sahihi, mtu anayeomba hawezi kupata Chakula cha Msingi. Ikiwa mtu atatoa taarifa ambayo anajua sio sahihi, anaweza kushtakiwa kwa kosa hilo. Adhabu za kuvunja kanuni za Chakula cha Msingi kwa makusudi ni tofauti, kuanzia kuvuliwa sifa ya programu, mpaka faini, au uwezekano wa kifungo.
- **Ikiwa utauza, utajaribu kuuza, utabadilishana au utachangia msaada wako wa chakula** kwa kitu chochote cha thamani kama vile fedha taslimu, dawa za kulevya, silaha, au kitu kingine chochote mbali na chakula kutoka kwa muuzaji wa rejareja aliyeidhinishwa (biashara haramu), unaweza kuvuliwa sifa ya kupokea ruzuku za msaada wa chakula kwa kiwango cha chini cha mwaka mmoja mpaka kiwango cha juu cha kuvuliwa sifa maisha yote kwa kosa la kwanza. Uvuliwaji huu wa sifa utaendelea hata kama utaondoka Jimbo la Washington na uombe ruzuku kwenye jimbo lingine.
- **Ikiwa utahitajika kushiriki katika masharti ya kazi ya Chakula cha Msingi**, na ukashindwa kushiriki, unaweza kuzuiwa kwa mwezi mmoja na hadi utakapotimiza mahitaji ya kazi kwa kushindwa kwa mara ya kwanza; miezi mitatu na hadi utakapotimiza kwa kushindwa kwa mara ya pili; na miezi sita na hadi utakapotimiza kwa mara ya tatu na kila wakati baada ya hapo.
- **Unaweza kuondolewa kwenye mpango wa Chakula cha Msingi** kwa kuvunja kanuni za mpango wa Chakula cha Msingi kama ilivyoelezwa kwenye onyo la adhabu ya Chakula cha Msingi iliyoorodheshwa kwenye ukurasa huu.
- **Ripoti matumizi ya kaya kama unataka idara iingize gharama hizi kwa ajili ya Chakula cha Msingi.** Ikiwa hutaripoti na kutoa ushahidi wa matumizi haya, hivyo unatamka kwamba hutaki tutumie matumizi haya ili kuamua kama unaweza kupata Chakula cha Msingi cha ziada.

Mambo Unayopaswa Kujua (Fedha Taslimu - TANF)

Kwa kupata Msaada wa Muda wa Familia Maskini (TANF) unakabidhi haki za msaada wa mtoto na mwenza wako kwenye Kitengo cha Msaada wa Mtoto. Hii inamaanisha kwamba DCS inaweza kuzuia usaidizi (madeni ya nyuma) ambavyo huongezeka unapopokea TANF. DCS itakutumia usaidizi wa sasa uliokusanywa wakati unapokea TANF.

- **Unalazimika kuwaeleza DCS haraka sana kama ulipokea malipo ya msaada wa mtoto au ruzuku** kwa ajili ya mtoto ulipokuwa TANF.
- **Ikiwa utacha kupokea TANF** utalazimika kuiambia DCS kuhusu mabadiliko yoyote yanayoathiri huduma ya watoto, kama vile mtoto haishi tena na wewe au anwani yako itabadilika.
- **Ikiwa utapata TANF, unaweza kuomba fedha ya ziada** kwa ajili ya kusaidia kulipa gharama za makazi ya muda ya dharura.

Mambo Unayopaswa Kujua (Fedha Taslimu - RCA)

Kwa kupata Msaada wa Fedha taslimu kwa Wakimbizi (RCA):

- **Unapaswa kuwa ni mseja au mwana-ndoa ambae hana watoto katika kaya.** Unapaswa utuambie ikiwa umekuwa ni mjamzito au unapaswa kumlea mtoto kwa sababu unaweza kustahiki proramu tofauti ya ruzuku ya fedha taslimu.
- **Unastahiki kupokea Msaada wa Fedha taslimu kwa Wakimbizi hadi miezi 4** kulingana na hali yako ya uhamiaji na tarehe uliyostahiki kupata programu na huduma za wakimbizi za serikali kuu.
- **Unapaswa kushiriki katika huduma za ajira na mafunzo** ndani ya siku 30 baada ya kupokea msaada, ambazo zinaweza kujumuisha shughuli za kukusaidia kupata kazi au kujifunza Kiingereza. Huenda usilazimike kushiriki katika huduma hizi ikiwa una ulemavu mkubwa au sugu, au unalazimika uwe nyumbani ili kumtunza mtu mzima mwengine mwenye ulemavu, au una umri wa miaka 60 au zaidi, au wewe ni mhanga wa ukatili wa kifamilia.
- **Kama sehemu ya masharti ya kupata huduma za ajira na mafunzo**, utapaswa kuhudhuria mahojiano yote ya kazi, kukubali ofa za kazi zinazofaa (isipokuwa ikiwa ni kinyume na makubaliano ya chama cha wafanyakazi ambacho wewe ni mwanachama au kazi hiyo ipo wazi kwa sababu ya mgogoro wa wafanyakazi), na huwezi kuacha kazi bila sababu ya msingi, kama inavyoamuliwa nasi.
- **Una haki ya kupata huduma nzuri za kazi na ajira na mafunzo.** Huduma zote za kazi na ajira na mafunzo lazima ziwe salama, bila ubaguzi, zijumuishe shughuli zilizo ndani ya wigo wa mpango wako wa huduma ya ajira / elimu na ambazo unaweza kufanya mara kwa mara, zihusishe saa za kawaida kwa kazi, na ziwe ndani ya muda unaofaa wa kusafiri (sio zaidi ya saa mbili au kama vile inavyokubalika katika eneo hilo). Huduma za mafunzo lazima ziwe na uwezo wa kukuongoza kupata kazi na mishahara inapaswa ifikie au kuzidi mshahara wa chini kabisa au haipaswi kuwa chini zaidi ya ile ambayo hulipwa kawaida kwa kazi kama hiyo.
- **Ikiwa utahitajika kukubali ofa ya kazi au kushiriki katika huduma za ajira na mafunzo za RCA**, na ukashindwa kufanya hivyo, msaada wako utasimamishwa au kupunguzwa. Punguzo ni miezi mitatu kwa kutoshiriki kwa mara ya kwanza na miezi sita kwa kila kutoshiriki baada ya hapo.
- **Unapaswa kuturipoti mapato yoyote ikiwa utapata kazi** hadi kufika tarehe 10 ya mwezi unaofuata.
- **Ukiwa wewe ni mlemavu, kipofu, au una umri zaidi ya miaka 65**, unaweza kupokea RCA unapoomba programu zingine za msaada na Utawala wa Usalama wa Jamii (SSA). Tutakusaidia kufanya maombi ya programu hizo. Mara tu ukiidhinishwa kupata programu ya msaada na SSA, ruzuku zako za RCA zitakoma.
- **Huwezi kupata RCA** ikiwa, ndani ya siku 30 kabla ya maombi yako uliacha kazi yako au ulikataa ofa nzuri ya kazi bila sababu ya msingi.

Taarifa ya Haki za Kiraia na Kutobagua

Kwa mujibu wa sheria ya haki za kiraia ya serikali kuu na kanuni na sera za haki za kiraia za USDA, USDA, na mashirika yake, ofisi zake, wafanyakazi wake, na taasisi zinazoshiriki au kusimamia programu za USDA zimepigwa marufuku kubagua kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, dini, jinsia, ulemavu, umri, hali ya ndoa, hali ya familia/nasaba, mapato yanayotokana na programu ya msaada kwa umma, imani za kisiasa, au kulipa kisasi au kulipiza kisasi kwa shughuli za awali za haki za kiraia, katika programu au shughuli yoyote inayofanywa au kufadhiliwa na USDA (sio misingi yote hutumika katika programu zote). Tarehe za mwisho za kuwasilisha malalamiko na suluhu zinatofautiana kulingana na programu au tukio husika.

Watu wenye ulemavu ambao wanahitaji njia mbadala za mawasiliano kwa ajili ya taarifa za programu (kwa mfano, Braille, maandishi makubwa, kanda ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani, n.k.) wanapaswa kuwasiliana na shirika la jimbo au la ndani linalosimamia programu hiyo au kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Mawasiliano ya Simu kwa 711 (ya sauti na TTY). Kwa kuongezea, taarifa ya mpango inaweza kupatikana kwa lugha nyingine isiyokuwa Kiingereza.

Kwa kutuma malalamiko ya kubaguliwa kwenye programu, jaza Fomu ya Malalamiko ya Kubaguliwa kwenye Programu ya USDA, AD-3027, inayopatikana mtandaoni katika Jinsi ya Kutuma Malalamiko ya Kubaguliwa kwenye Programu na katika ofisi yoyote ya USDA au andika barua na kuielekeza kwa USDA na toa katika barua hio taarifa zote zilizoombwa katika fomu hiyo. Kwa kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, piga simu (866) 632-9992. Tuma fomu yako iliyojazwa au barua kwenda USDA kwa:

1. **Tuma kwa posta**: USDA Food and Nutrition Service, 1320 Braddock Place, Room 334 Alexandria, VA 22314; au
2. **Barua pepe**: FNSCIVILRIGHTSCOMPLAINTS@usda.gov.

Sheria hii ni mtoa huduma wa fursa sawa.

Kwa kutia saini hapo chini, natamka kwamba nimepata haki zangu na majukumumu ya kupokea ruzuku za DSHS na programu nilizoelezewa. Naelewa kwamba ikiwa nitakataa kusaini nyaraka hii haitaathiri ustahiki wangu, lakini bado nawajibika na masharti ya programu na nitahusika na adhabu stahiki za programu au za jinai zinazotumika.

Saini ya Mwombaji Tarehe	Saini ya Mshirika wa Mwombaji Tarehe

ACES ID YA Mtumishi wa DSHS: ☐ Amekataa kusaini.